JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barabara ya Moshi Nairobi
S. L.P 1055
23103 ARUSHA
Barua pepe: **rbcarusha@pccb.go.tz**
Wavuti : www.pccb.go.tz

ARUSHA – JULAI 1, 2019

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU YAMNUSURU MTOTO ALIYENYIMWA NAFASI YA MASOMO YA SEKONDARI NA KUTAKIWA KUMSAIDIA MZAZI WAKE KUCHUNGA NG'OMBE

Katika mashauri yaliyotolewa uamuzi katika kipindi cha Aprili 2019 –Juni 2019, shauri la jinai Na. 28/2019 lilihusu mzazi mmoja aitwaye VICTORIA TARMO LOHAY ambaye alitoa hongo kwa afisa Mtendaji Kata ya Mang'ola ili asimfuatilie kwa mara ingine kwa kutomuhudhurisha mtoto shuleni ambaye awali alishtakiwa na afisa mtendaji wa Kata ya Mang'ola katika mahakama ya mwanzo Mang'ola kwa kushindwa kutii maelekezo ya serikali ya awamu ya tano ya kuhakikisha wazazi ambao watoto wao wamefaulu kuingia kidato cha kwanza wanawahudhurisha shuleni watoto wao na alitiwa hatiani na kulipishwa faini ya shilingi 50,000/ na kisha kutakiwa kumuhudhurisha mtoto wake aitwaye Paulo Qwande Slaqwe shuleni, aliyefaulu kutoka shule ya msingi Kisimagenda kwenda kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Domeli ziliyopo Wilaya ya Karatu.

Awali ilibainika kwamba licha ya kufaulu kuingia Shule ya Sekondari, mtoto huyo hakwenda kuripoti katika shule husika na hivyo mtendaji huyo alichukua hatua ya kuwafuatilia tena watoto ambao hata baada ya wazazi wao kulipishwa faini bado hawakuhudhurisha shule, ndipo siku moja kabla ya msako wa pili wa viongozi wa kata na kijiji mama huyo alifika katika ofisi ya mtendaji wa kata ya Man'gola ili kutoa hongo ya shilingi 20,000/ ili mtoto wake asihudhurishwe shuleni bali abaki kushiriki katika

shughuli za kifamilia za kuchunga ng'ombe. Baada ya kuona hali hiyo Mtendaji Bw. Petro Ngarikoi alitoa kwa haraka taarifa kwa TAKUKURU na kumnasa mzazi husika. Hivyo mzazi huyo alikutwa na hatia mbele ya Mhe. Isa_haq Kuppa hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama ya Wilaya ya Karatu na TAKUKURU ilimnusuru mtoto huyo na hatimaye kupata nafasi ya kuendelea na masomo kama watoto wenzake katika shule aliyochaguliwa.

Ndugu Wanahabari;

Kwa kipindi tajwa TAKUKURU (M) wa Arusha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 kama ifuatavyo;

1. **UCHUNGUZI NA MASHITAKA :**

   A. TAARIFA ZILIZOPOKELEWA

   Kwa kipindi tajwa zilipokelewa taarifa **149** kutoka sekta mbalimbali kama ilivyo katika jedwali lifuatalo;

Na	SEKTA	IDADI
1	Halmashauri	29
2	Elimu	8
3	Mahakama	14
4	Polisi	19
5	Ardhi	3
6	Afya	10
7	Kilimo	2
8	Zimamoto	1
9	NIDA	1
10	uhamiaji	1
11	Maji	1
12	NSSF	5
13	NCAA	5
14	Huduma za jamii	4
15	TANESCO	4
16	TANROAD/TARURA	5
17	TRA	4
18	Vyama vya ushirika	1
19	Dini	4
20	Tamisemi	5
21	Binafsi	15
22	Idara ya Kazi	5
23	Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali	1
JUMLA		**149**

Taarifa hizi zilipelekea kufunguliwa kwa majalada 42 ya Uchunguzi na yanaendelea kuchunguzwa na chunguzi zake zipo katika hatua mbalimbali. Pia ushauri yakinifu umekuwa ukitolewa kwa watoa taarifa kwa malalamiko yanayoonekana kutoangukia kwenye sheria yetu.

B. KESI MAHAKAMANI

Kwa kipindi tajwa, TAKUKURU (M) Arusha imefungua mashitaka mapya kumi na moja (11) mahakamani ambapo hadi sasa jumla ya mashauri arobaini (40) yanaendelea mahakamani yakiwa katika hatua mbalimbai za kimahakama.

Pia kwa kipindi hicho mashauri saba (7) yalitolewa uamuzi na kati yake Jamhuri imeshinda Mashauri Manne (4).

2. UFUATILIAJI WA FEDHA ZA UMMA KWENYE MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU (M) wa Arusha kwa kipindi tajwa imefanya ufatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika miradi kumi na tisa (19) ambayo serikali imewekeza fedha kiasi cha **Sh. 15, 338,365,374/=** na **USD 1,011,808.12**. Miradi hiyo imefuatiliwa ipo katika hatua mbalimbali na thamani ya fedha (Value for Money) ipo. ***Rejea kiambatisho "A"***

3. ELIMU KWA UMMA:

TAKUKURU (M) Arusha imeendelea kufanya jitihada za kuelimisha Umma juu ya uelewa mpana wa dhana ya Rushwa na pia kuwakumbusha wajibu wao katika mapambano dhidi ya Rushwa. Kama inavyofahamika kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi hivyo elimu yetu imejikita sana katika kuuelimisha umma na juu ya wajibu wao wa kuchagua viongozi wanaofaa na sio watoa Rushwa.

Katika kipindi tajwa jumla ya wananchi **8,865** wamefikiwa ikiwa wanaume ni **4,810** na wanawake ni **4,058** kwa njia zifuatazo;

Na	KAZI ILIYOFANYIKA	IDADI
1	SEMINA	14
2	MIKUTANO/MIJADALA	28
3	KUFUNGUA KLABU	43
4	KUIMARISHA KLABU	210
5	MAONYESHO	5
6	UANDISHI WA MAKALA	5
7	TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI	1
8	UGAWAJI WA VIPEPERUSHI MBALIMBALI	1,120

4. FEDHA ZILIZOOKOLEWA

TAKUKURU (M) wa Arusha katika kipindi cha Mwezi Aprili – Juni 2019, imefanikiwa kuokoa fedha na mali za serikali zenye thamani ya jumla kiasi cha **Sh.** 1**52,326,943/=** katika sekta ya Afya, Elimu na Ardhi. Fedha hizo ambazo tulizibaini ubadhirifu wake baada ya kufanya Uchunguzi zimeokolewa na kurudishwa serikalini. Katika fedha hizo kulikuwa na **Sh. 118,202,943/=** zilikuwa ni mishahara hewa, **Sh. 960,000/=** zikiwa ni posho zilizolipwa kinyume na stahiki kwa wahusika, na **Sh. 33,200,000/=** ikiwani ni thamani ya kiwanja kilichorudishwa serikalini baada ya uchunguzi kubaini kiwanja hicho kilichouzwa kwa bei ya chini ya soko yaani Milion 11 na kinyume na utaratibu.

5. MWELEKEO WETU KWA MWAKA 2019/2020

Ndugu Wanahabari;

TAKUKURU (M) wa Arusha kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka mpya wa fedha (2019/2020) tumejizatiti kwa kufanya yafuatayo;-

- Kuelimisha wananchi makundi yote juu ya wajibu wao katika mapambano Dhidi ya Rushwa na hasa kujikita katika kutoa elimu ya Rushwa katika Uchaguzi na madhara ya viongozi wanaopatikana kwa njia ya Rushwa.

- Kufanya **Utafiti/ uchambuzi wa mifumo katika sekta ya ukusanyaji mapato** katika ukadiriaji kodi unaofanywa na halmashauri na Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA, **kufanya udhibiti katika miradi ya maji na ukusanyaji mapato**, ufuatiliaji katika miradi ya elimu inayoendelea kutekelezwa katika Mkoa wa Arusha.

- Kufanya ufuatiliaji wa Rushwa kipindi chote cha uchaguzi kuanzia kwenye kampeni mpaka siku ya kupiga kura.

- Kuendelea kutafuta na kupokea taarifa za vitendo vya Rushwa vinavyofanywa na watu mbalimbali ikiwa ni watumishi wa umma, viongozi mbalimbaliau watu binafsi na kuwafikisha mahakamani wote watakaobainika na hatia.

6. MWISHO

Ndugu Wanahabari;

TAKUKURU (M) wa Arusha tunawashukuru kwa ushirikiano kwa kipindi chote cha mwaka 2018/2019 kwani ushirikiano wenu umekuwa na tija sana katika utendaji kazi wetu kwani wananchi wengi wamesikia na kusoma habari zetu kupitia vyombo vyenu. Hivyo tunaomba msichoke kuendelea kutuunga mkono katika jitihada hizi za mapambano dhidi ya Rushwa kwani jukumu hili ni zito na tukiachiwa TAKUKURU pekee hatutafanikiwa.

Pia tunawashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wao na tunazidi kutoa wito kwao kuendelea kushirikiana na TAKUKURU kwa kuwafichua wale wote wanaojihusisha na vitendo vya Rushwa.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawaonya watu wote na watumishi wa Umma wanaotumia nafasi zao kujipatia manufaa wasiostahili na hivyo kuisababishia serikali hasara kuacha kufanya hivyo mara moja vinginevyo watakutana na mkono wa sheria. Na tunawaasa wananchi kutokubali kununuliwa katika kipindi hiki cha uchaguzi kwa kuwa viongozi wanaopatikana kwa njia za Rushwa hawafai na hawaitakii mema nchi yetu.

Kataa Rushwa, Jenga Tanzania

Asanteni kwa kunisikiliza

Imetolewa na:

FRIDA WIKESI,
MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA
……..